

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM


**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com




## MATANGAZO: DOMINIKA 30 YA MWAKA C - 26.10.2025

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA 26.10.2025 | **DOMINIKA YA 30 YA MWAKA C WA KANISA**<br><br>Mchango wa pili kwa ajili ya Utume wa Familia. |
| 2. | JUMANNE 28.10.2025 | Sikukuu ya Watakatifu Simoni na Yuda Thadei, Mitume |
| 3. | JUMATANO 29.10.2025 | Siku ya mapumziko ya kazi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu. Tuendelee kuombea nchi yetu |
| 4. | JUMAMOSI 01.11.2025 | Kutakuwa na Misa ya kuhitimisha matembezi ya Sanamu ya Bikira Maria katika **Kanda F na G** saa 1:00 asubuhi na kukabidhi Sanamu kwa **Kanda H**. Jumuiya zihimize na kufuatilia bahasha za Kapu la Mama na kuzirejesha katika Misa za kuhitimisha matembezi ya sanamu. |
| 5. | JUMAMOSI 01.11.2025 | Sherehe ya Watakatifu Wote na Jumamosi ya kwanza ya mwezi. Misa Parokiani saa 3:00 asubuhi. Wasimamizi ni WAWATA |
| 6. | DOMINIKA 02.11.2025<br><br>DOMINIKA YA KWANZA YA MWEZI, ZAKA NA KILELE CHA MAVUNO PAROKIA<br>- MISA MOJA TU | **KUMBUKUMBU, KUWAOMBEA WAAMINI MAREHEMU WOTE**<br><br>**Misa moja tu : Saa 1:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Katarina wa Siena na Mt. Yohane Mbatizaji<br>Watangaza Neno: Leticia Shija na Mary Mbowe<br><br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya ujenzi. |
| 7. | HITIMISHO LA MAVUNO PAROKIA 2025 | Tulizindua Mavuno Parokia 05.10.2025 na waamini kuahidi mavuno yao ya 2025. Viongozi wa Jumuiya wanatakiwa kufuatilia familia ambazo hazijaahidi na walioahidi kukamilisha kabla ya siku ya kilele Dominika ijayo 02.11.2025. Wenye mavuno ya vitu waviorodheshe na bei yake kwa viongozi wa Jumuiya na viletwe siku hiyo ambapo utafanyika mnada wa vitu. Kilele cha Mavuno Jimbo ni Jumamosi 22.11.2025 ambapo tutawasilisha taarifa ya Parokia na kushiriki sote |
| 8. | VITI VYA PAROKIA | Leo ndiyo mwisho wa Jumuiya zinazohitaji viti kufanya taratibu za malipo ili viweze kununuliwa viti vipya. |
| 9. | UCHAGUZI WA VIONGOZI WA KANDA | Kanda zilizofanya chaguzi za Vyama vya Kitume zinatakiwa kuwasilisha fomu za matokeo, na chaguzi zilizobakia viongozi wa Kanda watafute utaratibu wa kukamilisha. **Uchaguzi wa Kamati Tendaji za Kanda utafanyika Jumamosi 08.11 na 15.11.2025**. |

| | | |
|---|---|---|
| 10. | KUWAOMBEA MAREHEMU | Mwezi Novemba ni mwezi wa kuwakumbuka na kuwaombea marehemu wetu. Fomu za kuwaombea zitatolewa wiki ijayo na tutatakiwa kuweka sadaka ya nia ya kuwaombea katika Misa. Fomu na sadaka ziwekwe kwenye bahasha na kufungwa. |
| 11. | HUDUMA YA AFYA NA USHAURI WA SHERIA | Kutakuwa na huduma ya kupima afya na ushauri, pamoja na ushauri wa kisheria hapa Parokiani Dominika ya 09.11.2025 kupitia wataalamu wetu wa Parokia bila gharama kwa waamini. Huduma itaanza kutolewa mara baada ya Misa ya kwanza. |
| 12. | HIJA YA WALIMU WAKATOLIKI WOTE JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM | Umoja wa Wakatoliki Jimbo Kuu la Dar unawatangazia walimu Wakatoliki wote kuanzia ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu (waliopo kazini na waliostaafu) kuwa na Hija ya Pamoja itakayofanyika Jumamosi ijayo 01.11.2025 katika kituo cha Hija Pugu kuanzia saa 3:00 asubuhi. Hii ni sehemu ya Hija za makundi katika mwaka wa Jubilei Kuu. Vazi rasmi la Hija ni kitenge cha walimu wakatoliki kinachopatikana kwa Sh. 35,000/=. |
| 13. | MATANGAZO YA KWAYA | Kwaya ya Mt. Yohane Paulo II leo wanasherehekea sikukuu ya Msimamizi wao, na watashiriki kuimba katika Misa ya 1 na ya 2.<br><br>Kwaya ya Vijana ya Kung'ara kwa Yesu Kristo leo wanafanya ziara ya kuinjilisha katika Kituo cha Malezi Child in the Sun, Makabe. |
| 14. | MAREJESHO YA VITABU | Jumuiya zinakumbushwa kufanya malipo ya vitabu vya Liturujia ya Sikukuu ya sikukuu ya Parokia tarehe 10.08.2025. |
| 15. | KIKAO CHA WANAUME WOTE | Kutakuwa na kikao kifupi cha wanaume wote leo mara baada ya Misa ya kwanza. |
| 16. | WARSHA YA WAAMINI WOTE JIMBO | Warsha ya waamini wote wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam itafanyika Jumamosi 29.11.2025 katika viwanja vya Parokia ya Kristo Mfalme Tabata kuanzia saa 2:00 asubuhi. Kutakuwa na Mada mbili,<br>1. Uchaguzi/Uongozi katika Kanisa 2. Mwaka wa Jubilei Kuu<br>Kutakuwa pia na vyeti kwa wenye Jubilei za miaka 25, 50 na 75.<br>**Sasa ada ya ushiriki imeondolewa, ushiriki ni bure, tujiandikishe kwa wingi.**<br>***Kila Jumuiya inatakiwa kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya uandikishaji washiriki wa Warsha kwani inatakiwa Jimboni.*** |
| 17. | CHAKULA KWA WAHITAJI | Chakula kwa wahitaji kitatolewa Jumanne, 28.10.2025 saa 10:00 jioni. Wahusika wafike kwa wakati. |
| 18. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini Letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kauli Mbiu ya Mwaka wa Jubilei Kuu: "Jubilei 2025 – Mahujaji wa Matumaini."***

**MATEMBEZI YA SANAMU YA BIKIRA MARIA KATIKA MWEZI WA ROZARI NA KAMPENI YA KAPU LA MAMA MARIA 2025**

| WIKI | TAREHE | KANDA HUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | 28/09 - 04/10 | A |
| 2 | 04/10 – 11/10 | B |
| 3 | 11/10 – 18/10 | C |
| 4 | 18/10 – 25/10 | D & E |
| 5 | 25/10 – 01/11 | F & G |
| 6 | 01/11 – 08/11 | H |
| 7 | 08/11 – 15/11 | I |
| 8 | 15/11 – 22/11 | J |
| 9 | 22/11 – 29/11 | K |

**MATANGAZO NDOA KWA MARA YA PILI**

1. Frank Samwel Mruma BIN Samwel Simon Mruma na Maria Rajabu Mchomvu wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

Anatarajia kufunga ndoa na:

Lightness Anold Mariki BINTI Anold Yohane Mariki na Kristina Makyao wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

2. Nobert Alfons Matage BIN Alfons Matage na Theodosia Mbanga wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

Anatarajia kufunga ndoa na:

Anna Raphael Mngazija BINTI Raphael Mngazija na Aisha (Suzana) Ramadhani wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

**MASOMO DOMINIKA – KUMBUKUMBU YA MAREHEMU WOTE - 02.11.2025**

| | |
|---|---|
| SOMO I | Hek 3:1-9 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 23 |
| SOMO II | Rum 6:3-9 |
| SHANGILIO | |
| INJILI | Mt 25:31-46 |